

SwahiliWeb

ELECTRONIC DEPOSITORY AND RESOURCE ARCHIVE

www.swahiliweb.net

Archive: Pat Caplan

Document: Unknown man (Swahili)

File reference: SW/PC/13036

This document has been downloaded from the SwahiliWeb archive on the understanding that it is copyright under the laws of the United Kingdom and the Berne Convention, and that no further copying, storage or distribution, in any form or by any means, including electronically, is permitted except under the provisions of fair dealing.

Copyright of all materials deposited with SwahiliWeb remains with the copyright holder. Those seeking copyright and associated permissions will be referred to the copyright holder.

**Interview in Kanga village 1985 with Unknown Man
transcribed 1210 by Joseph Bwathondi in 2010**

PAT: Umezaa watoto wangapi?

UM: Kwa sasa hivi amaezaa watoto wakike kama nne.

PAT: Umeshapata na wajukuu

UM: Ndio na mmoja wao ni huyu hapa, wengine wapo na mama zao.

UM: Je mama umepata watoto?

PAT: Ndio wawili.

UM: Mbona husije nao?

PAT: Haa inakuwa tabu nauli kubwa na wao wanasoma shule.

UM: Hivyo. Wapo daresa la ngapi?

PAT: La nane na la tisa

UM: Kule hakuko kama kwetu ukimaliza darasa la saba ndio mwisho?

PAT: Ah huku si ukimaliza la saba si unaingia sekondari.?

UM: Lakini si mpaka mtu afaulu kuendelea?

PAT: Kwa sisi lazima uendelee mpaka ukifika miaka 16

UM: Sawa sawa

PAT: Hawana ruhusu ya kutoka shule.

UM: Tanzania baada ya miaka saba basi.

PAT: Najua, lakini wanapopasi wataweza kuendelea .

UM: Sasa utakuta watoto wanatoka darasa la saba hata kazi hawaziwezi. Sasa kama huyu amemaliza darasa la saba je ataaminika kupewa kazi?.

PAT: Kwani huyu ana umri gani?

UM: Kama miaka kumi na nne

PAT: Anafanya kazi gani

UM Hafanyi kazi yoyote ile yaani tunavua tu. Kamaliza la saba.

PAT: Hajaenda Dar es Salaam?

UM: Hajaenda

PAT: Anataka kwenda

UM: Ndio.

PAT: wewe unasemaje?

UM: Aende lakini kwenda kwake akakae na mtu. Sio mwenyewe

PAT: Huna jamaa Dar es salaam?

UM: Sina ninao Uguja

PAT: Kazi gani inapatikana Uguja?

UM: Uguja ni kazi kazi tu hizo za, ukarani wa makampuni ukarani wa mashirika, viwandani.

PAT: Kazi ya Karafuu hakuna?

UM: Karafuu, unaulizia aende kwenye karafuu?

PAT: Ndio.

UM: Karafuu ni kazi ya mwaka (kazi ya msimu)

PAT: Kazi inayofanyika kulingana na msimo wa mwaka

UM: Kama kazi ya kuvuna mpunga sio wakati wa kuvuna mtu yoyote anakwenda. Ndio nilipoamua bora akae hapa.

PAT: Ndio

UM: Na tutavua na tunavua

PAT: Sasa samaki unaiza hapa au unapeleka wapi?

UM: Ninapeleka Ng'onda halafu anapopatikana mchuuzi tunawauzia au tunaenda wenyewe sokoni. Mbona wapo jamaa tu wengi

PAT: Hivyo

UM: Mzee Pwagu yupo Mama Pwagu yupo

PAT: Eh nawajua sana

UM: Mzee

PAT: Lakini kazi hana

UM: Anafanya kazi ya kulipwa

PAT: Baba yake mkubwa Daudi Makame

UM: Eh. Baba yake mkubwa Daudi anaitwa Selemani

PAT : Haujasikia? Huyu amepata kazi ya sh 7,000.00

UM: Kazi vipi bado?

PAT: Kazi sijasikia ikitangazwa kama watapata kazi tena au la. Lakini watakuja hivi karibuni.

UM: Watakuja?

PAT: Watakuja kukaa zaidi hapa.

UM: Salim mlionana

PAT: Tulionana Dar es salaam.

UM: Mlionana nae wapi Dar es salaam?

PAT: Alikuja kunipokea uwanja wa ndege nilipotua kutoka London

UM : Kwani kutokea London kwa ndege mpaka Dar es salaam mnachukua muda gani

PAT: Siku moja tu. Kutwa unakwenda.

UM: Hivi hizo ni ndege kubwa

PAT: Ndio.

UM: Kama hizi zinazopitapita usiku?

PAT: Ndio na hizi ndege zinakwenda mbio kweli kweli kuliko hizi zinazotoka Dar es salaam. Nkwenda Kilindoni

UM: Je hizi zinaweza kufika Londani

PAT: Kufika Londani haziwezi kufika

UM: Ndege hizi ni za kwenda Mafia , Dar es salaam, ziende hapo Nairobi

PAT: Pengine , lakini manake ni ndege ndogo

UM: Kwani zile ndege zinatengenezwa je

PAT: Ndege hizi kubwa?

UM: Zile ndogo

PAT: Zinatengenezwa (Some words are missing).....

UM: mpaka atoe taarifa Mwarabu Yule, mpaka kuanza na kupiga picha.

PAT: Mpaka huko wapi?

UM : huko Israeli, kwa myaudi Yule sijuhi kabila gani. Lakini bahati haikuwa yangu baada ya watu kufanya fitina pale na ndio ikawa mwisho wangu na akachukuliwa mtu mwingine.

PAT: Mh!

UM : Ningekuwa kule sasa... (*Recording in this part is very poor and words not distinguishable*)

PAT: Huyu ni mtoto wako?

UM: Ndio na ameshakwisha kuolewa

PAT: Je ana watoto?

UM: Lakini watoto bahati mbaya.

PAT: Eh! Haya basi nakwenda zangu.

UM: Karibu.